

SWAHILI	ENGLISH
TITO 1	TITUS 1
1:1 Paulo, mtumwa wa Mungu, na mtume wa Yesu Kristo; kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu, na ujuzi wa kweli ile iletayo utauwa;	1 Paul, a servant of God and an apostle of Jesus Christ for the faith of God's elect and the knowledge of the truth that leads to godliness—
1:2 katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele;	2 a faith and knowledge resting on the hope of eternal life, which God, who does not lie, promised before the beginning of time,
1:3 akalifunua neno lake kwa majira yake katika ule ujumbe niliowekewa amana mimi kwa amri ya Mwokozi wetu Mungu;	3 and at his appointed season he brought his word to light through the preaching entrusted to me by the command of God our Savior,
1:4 kwa Tito, mwanangu hasa katika imani tuishirikiyo. Neema na iwe kwako na amani zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Mwokozi wetu.	4 To Titus, my true son in our common faith: Grace and peace from God the Father and Christ Jesus our Savior.
1:5 Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru;	5 The reason I left you in Crete was that you might straighten out what was left unfinished and appoint[a] elders in every town, as I directed you.
1:6 ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, ana watoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. –	6 An elder must be blameless, the husband of but one wife, a man whose children believe and are not open to the charge of being wild and disobedient.
1:7 Maana imempasa askofu a awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu;	7 Since an overseer[b] is entrusted with God's work, he must be blameless—not overbearing, not quick-tempered, not given to drunkenness, not violent, not pursuing dishonest gain.
1:8 bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake;	8 Rather he must be hospitable, one who loves what is good, who is self-controlled, upright, holy and disciplined.
1:9 akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga.	9 He must hold firmly to the trustworthy message as it has been taught, so that he can encourage others by sound doctrine and refute those who oppose it.
1:10 Kwa maana kuna wengi wasiotii, wenye maneno yasiyo na maana, wadanganyaji, na hasa wale wa tohara, ambao yapasa wazibwe vinywa vyao.	10 For there are many rebellious people, mere talkers and deceivers, especially those of the circumcision group.
1:11 Hao wanapindua watu wa nyumba nzima, wakifundisha yasiyowapasa kwa ajili ya mapato ya aibu. –	11 They must be silenced, because they are ruining whole households by teaching things they ought not to teach—and that for the sake of dishonest gain.

SWAHILI	ENGLISH
1:12 Mtu wa kwao, nabii wao wenyewe, amesema, Wakrete ni waongo siku zote, hayawani wabaya, walafi wavivu.	12 Even one of their own prophets has said, "Cretans are always liars, evil brutes, lazy gluttons."
1:13 Ushuhuda huo ni kweli. Kwa sababu hiyo uwakemee kwa ukali, ili wapate kuwa wazima katika imani;	13 This testimony is true. Therefore, rebuke them sharply, so that they will be sound in the faith
1:14 wasisikilize hadithi za Kiyahudi, wala maagizo ya watu wajiepushao na yaliyo kweli. –	14 and will pay no attention to Jewish myths or to the commands of those who reject the truth.
1:15 Vitu vyote ni safi kwa hao walio safi; lakini hakuna kilicho safi kwao walio wanajisi, wasioamini; bali akili zao zimekuwa najisi, na nia zao pia. –	15 To the pure, all things are pure, but to those who are corrupted and do not believe, nothing is pure. In fact, both their minds and consciences are corrupted.
1:16 Wanakiri ya kwamba wanamjua Mungu, bali kwa matendo yao wanamkana; ni wenye machukizo, waasi, wala kwa kila tendo jema hawafai. –	16 They claim to know God, but by their actions they deny him. They are detestable, disobedient and unfit for doing anything good.
TITO 2	TITUS 2
2:1 Lakini wewe nena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima;	1 You must teach what is in accord with sound doctrine.
2:2 ya kwamba wazee wawe wenye kiasi, wastahivu, wenye busara, wazima katika imani na katika upendo na katika saburi. –	2 Teach the older men to be temperate, worthy of respect, self-controlled, and sound in faith, in love and in endurance.
2:3 Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingizaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema;	3 Likewise, teach the older women to be reverent in the way they live, not to be slanderers or addicted to much wine, but to teach what is good.
2:4 ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao;	4 Then they can train the younger women to love their husbands and children,
2:5 na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe.	5 to be self-controlled and pure, to be busy at home, to be kind, and to be subject to their husbands, so that no one will malign the word of God.
2:6 Vivyo hivyo na vijana waume uwaonye kuwa na kiasi;	6 Similarly, encourage the young men to be self-controlled.
2:7 katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu,	7 In everything set them an example by doing what is good. In your teaching show integrity, seriousness
2:8 na maneno yenye uzima yasiyoweza kuhukumiwa makosa, ili yule mwenye kupinga atahayarike, kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yetu.	8 and soundness of speech that cannot be condemned, so that those who oppose you may be ashamed because they have nothing bad to say about us.

SWAHILI	ENGLISH
2:9 Watumwa na wawatii bwana zao, wakiwapendeza katika mambo yote; wasiwe wenye kujibu,	9 Teach slaves to be subject to their masters in everything, to try to please them, not to talk back to them,
2:10 wasiwe waibaji; bali wauonyeshe uaminifu mwema wote, ili wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu katika mambo yote. –	10 and not to steal from them, but to show that they can be fully trusted, so that in every way they will make the teaching about God our Savior attractive.
2:11 Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa;	11 For the grace of God that brings salvation has appeared to all men.
2:12 nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa;	12 It teaches us to say "No" to ungodliness and worldly passions, and to live self-controlled, upright and godly lives in this present age,
2:13 tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu;	13 while we wait for the blessed hope—the glorious appearing of our great God and Savior, Jesus Christ,
2:14 ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomoe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.	14 who gave himself for us to redeem us from all wickedness and to purify for himself a people that are his very own, eager to do what is good.
2:15 Nena maneno hayo, onya na kukaripia kwa mamlaka yote; asikudharau mtu awaye yote. –	15 These, then, are the things you should teach. Encourage and rebuke with all authority. Do not let anyone despise you.
TITO 3	TITUS 3
3:1 Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema;	1 Remind the people to be subject to rulers and authorities, to be obedient, to be ready to do whatever is good,
3:2 wasimtukane mtu ye yote, wasiwe wagemvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote. –	2 to slander no one, to be peaceable and considerate, and to show true humility toward all men.
3:3 Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukiana. –	3 At one time we too were foolish, disobedient, deceived and enslaved by all kinds of passions and pleasures. We lived in malice and envy, being hated and hating one another.
3:4 Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa;	4 But when the kindness and love of God our Savior appeared,
3:5 si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;	5 he saved us, not because of righteous things we had done, but because of his mercy. He saved us through the washing of rebirth and renewal by the Holy Spirit,

SWAHILI	ENGLISH
3:6 ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu;	6 whom he poured out on us generously through Jesus Christ our Savior,
3:7 ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu. –	7 so that, having been justified by his grace, we might become heirs having the hope of eternal life.
3:8 Ni neno la kuaminiwa; na mambo hayo nataka uyanene kwa nguvu, ili wale waliomwamini Mungu wakumbuke kudumu katika matendo mema. Hayo ni mazuri, tena yana faida kwa wanadamu.	8 This is a trustworthy saying. And I want you to stress these things, so that those who have trusted in God may be careful to devote themselves to doing what is good. These things are excellent and profitable for everyone.
3:9 Lakini maswali ya upuzi ujiepushe nayo, na nasaba, na magomvi, na mashindano ya sheria. Kwa kuwa hayana faida, tena hayana maana. –	9 But avoid foolish controversies and genealogies and arguments and quarrels about the law, because these are unprofitable and useless.
3:10 Mtu aliye mzushi, baada ya kumwonya mara ya kwanza na mara ya pili, mkatae;	10 Warn a divisive person once, and then warn him a second time. After that, have nothing to do with him.
3:11 ukijua ya kuwa mtu kama huyo amepotoka, tena atenda dhambi, maana amejihukumu hatia yeye mwenyewe.	11 You may be sure that such a man is warped and sinful; he is self-condemned.
3:12 Wakati nitakapomtuma Artema kwako au Tikiko, jitahidi kuja kwangu huku Nikopoli; kwa maana huku nimekusudia kukaa wakati wa baridi. –	12 As soon as I send Artemas or Tychicus to you, do your best to come to me at Nicopolis, because I have decided to winter there.
3:13 Zena, yule mwana-sheria, na Apolo, uwasafirishe kwa bidii, wasipungukiwe na cho chote. –	13 Do everything you can to help Zenas the lawyer and Apollos on their way and see that they have everything they need.
3:14 Watu wetu nao wajifunze kudumu katika matendo mema, kwa matumizi yaliyo lazima, ili wasiwe hawana matunda.	14 Our people must learn to devote themselves to doing what is good, in order that they may provide for daily necessities and not live unproductive lives.
3:15 Watu wote walio pamoja nami wakusalimu. Tusalimie wale watupendao katika imani. Neema na iwe pamoja nanyi nyote.	15 Everyone with me sends you greetings. Greet those who love us in the faith. Grace be with you all.